

---

**KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL  
REVISION MOCK EXAMS 2016  
TOP NATIONAL SCHOOLS**

**MOI GIRLS SCHOOL - NAIROBI  
KISWAHILI  
KARATASI YA 3**

**SCHOOLS NET KENYA**  
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor  
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27  
E-mail: [infosnkenya@gmail.com](mailto:infosnkenya@gmail.com) | Website: [www.schoolsnetkenya.com](http://www.schoolsnetkenya.com)

---

---

# MOI GIRLS SCHOOL - NAIROBI KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

102/3

FASIHI

KARATASI YA TATU

SEHEMU A: USHAIRI.

---

1. Swali la lazima.

GANGA SHINA.

- |  |  |
|--|--|
| 1. Maradhi na taathira<br>Zimeshajiri ishara<br>Vitawi kuporapora<br>Ganga shina la uhai   | ya tego na ulemavu<br>za mti kuwa mbovu<br>mti wazidi ukavu<br>tanzuze hazigangiki     |
| 2. Karibu si masihara<br>Na magambo kuyapara<br>Haiji thama nusura<br>Ganga shina la uhai  | kwataka kutuma nguvu<br>hata viache koru<br>ukichelea mabivu<br>tanzuze hazigangiki    |
| 3. Makongwe yanayokera<br>Na mizizi ya safura<br>Usiwe nayo subira<br>Ganga shina la uhai  | yakate kwa maumivu<br>iliyo mikandamivu<br>katika utimilivu<br>tanzuze hazigangiki     |
| 4. Rasharasha sio bora<br>Imwailie imara<br>Uchome moto sangara<br>Ganga shina la uhai     | dawa iwe rovurovu<br>hadi isombe kitovu<br>mti uwe muangaru<br>tanzuze hazigangiki     |
| 5. Fyekafyeka miparura<br>Inayonyonya ujira<br>Nasaha zangu dharura<br>Ganga shina la uhai | mimea mitatagivu<br>wa miti mishughulivu<br>kesho utakula mbivu<br>tanzuze hazigangiki |

Maswali.

- a) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
- b) Mwandishi ametumia jazanda katika kueleza jambo fulani. Taja jazanda hiyo na ueleze maana yake. (alama 4)
- c) Mwandishi anamaanisha nini anaposema “Kutibu si masihara kwataka kutuma nguvu? (alama 2)
- d) Mwandishi ametumia inkisari. Taja mifano miwili na uandike inavyotakikana. (alama 2)
- e) Eleza maana ya kibwagizo cha shairi hili. (alama 2)
- f) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumiwa katika shairi hii; (alama 5)
- i) Kupora pora
-

- ii) Isombe
- iii) Sangara
- iv) Miparura
- v) mishughulivu.

**SEHEMU B: RIWAYA**

**K. Walibora: Kidagaa Kimemwozea.**

**Jibu swali la 2 au la 3.**

2. Dhuluma ni jambo la kawaida katika jumuiya ya Kidagaa Kimemwozea. Jadili. (alama 20)
3. "Huyu mwendawazimu anakuja nini kwenye sherehe hizi? Anafikiri sherehe hizi ni za watu wenye kichaa kama yeye?"
  - (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  - (b) Eleza tamathali mbili zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)
  - (c) Thititisha kuwa anayerejelewa ni mwendawazimu na vile vile si mwendawazimu. (alama 12)

**SEHEMU C: TAMTHILIA**

**Jibu swali la 4 au la 5.**

4. "Tuendelee kusonga mbele hatua kwa hatua. Bwana fedha na kazi ...."
  - (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  - (b) Taja sifa nne za anayesemewa. (alama 4)
  - (c) Baraza la Cheneo limeendelea kuwepo mamlakani kwa mbinu kadha . Jadili. (alama 12)
5. Hatua tuchukuazo maishani mwetu zaweza kutuathiri na kuathiri nchi pakubwa. Thibitisha kauli hii ukirejelea mhusika Meya Sosi. (alama 20)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

**K. Walibora na S. A Mohamed: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.**

**Jibu swali la 6 au la 7.**

6. "Shangazi wakumbuke watoto. Waonee huruma!"
  - (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
  - (b) Fafanua mbinu ya kisanaa inayojitokeza katika kauli hii. (alama 2)
  - (c) Jadili jinsi maudhui ya ukatili yameendelezwa na wahusika wengine katika hadithi (alama 6)
  - (d) Eleza sifa nne za anayerejelewa katika dondoo. (alama 8)
7. Mwimba wa kujichoma hauambiwi pole. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi zozote kumi. (alama 20)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI.**

8. (a) Maghani ni nini? (alama 2)
- (b) Eleza fani zifuatazo za maghani. (alama 4)
- i) Vivugo.
- ii) Tondozi
- iii) Pembezi
- iv) Rara
- (c) Eleza maana ya neno ULUMBI. (alama 1)
- (d) Bainisha sifa za mlumbi. (alama 6)
- (e) Eleza umuhimu wa ulumbi. (alama 3)